**ELIMIKA SECONDARY SCHOOL**
***P.O.BOX 818, SONGEA - TANZANIA***
***Email: wilolesi15@gmail.com***
***Mobile: +255 756 865 531, 766 067 838***
**REG. S.5271**

**NDUGU..........................................................**
**......................................................................**

# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ELIMIKA MWAKA 2025

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa katika shule ya Sekondari ya ELIMIKA iliyopo katika mtaa **MJIMWEMA**, kata ya **MJIMWEMA** . Shule ipo katika Manispaa ya Songea, mkoa wa Ruvuma Kilometa 2 kutoka Songea mjini katika barabara ya kuelekea Hospital ya MJIMWEMA. Hivyo tunapenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule ya **ELIMIKA** Sekondari. Nategemea utakuwa tayari kusoma, kutii na kuwa mfano bora katika kujifunza kwa wakati wote utakao kuwa katika masomo.

Shule ni ya jinsia zote **WAVULANA** na **WASICHANA**, Masomo yanayofundishwa ni **Basic Mathematics, Biology, Physcis, Chemistry, Civics, History, Geography, English Language, Kiswahili na Literature in English.**

Shule ina miundombinu itakayo mfanya mwanafunzi mda wote aweze kujifunza na kujiskia raha awapo shuleni, shule ina umeme, maji maktaba na maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi.

Shule itafunguliwa tarehe ***05 Januari 2025***, unatakiwa kuripoti tarehe iliyo tajwa bila kukosa.

## ADA YA SHULE KWA MWAKA

**A. WATAKAO KAA BWENI [SHULEN]**

- ❖ **ADA YA SHULE** NI TSHS **600,000**/=

**B. WATAKAO KAA NYUMBANI (DAY)**

- ❖ **ADA YA SHULE** SH, **600,000/=**

## MCHANGANUO WA ULIPAJI WA MICHANGO YA SHULE

| MWEZI | DOMITORY (BWENI) | DAY (KUTWA) |
|---|---|---|
| **JANUARI** | AWAMU YA I<br>**150000/=** | AWAMU YA I<br>**150000/=** |
| **APRILI** | AWAMU YA II<br>**150,000/=** | AWAMU II<br>**150,000/=** |
| **JULAI** | AWAMU YA III<br>**150,000/=** | AWAMU YA III<br>**150,000/=** |
| **SEPTEMBA** | AWAMU YA IV<br>**150,000/=** | AWAMU IV<br>**150,000/=** |
| | **JUMA KUU KWA MWAKA SH. 600,000/=** | **JUMLA KUU KWA MWAKA 600,000/=** |

## MICHANGO YA CHAKULA

**WATAKAOKAA BWENINI**

- ❖ Kwa mwanafunzi atakaye kaa Bwenini, mzazi/mlezi wa mwanafunzi atachangia chakula yaani dumla 30 (debe 6) za mahindi na maharage dumla 6 (debe 1 na kilo 4) na Mchele dumla 2 (kilo 8) kwa muhula (yaani ***mwezi wa kwanza hadi wa sita dumla 30 (sawa na debe 6) za mahindi, maharage dumla 6 (debe 1 na kilo 4), Mchele dumla 2 (kilo 8) na***

***mwezi wa saba hadi wa kumi na mbili dumla 30 (debe 6) za mahindi, mchele dumla 2 (kilo 8) na maharage dumla 6 (debe 1 na kilo 4))***

## WATAKAOKAA NYUMBANI

- Mzazi/mlezi atachangia chakula yaani dumla 20 (debe 4) na maharage dumla 4 (Kilo 16) kwa muhula

***MICHANGO MINGINE TOFAUTI NA ADA***

A. Rimu bunda mbili (januari 01 na julai 01)
B. Dharura kwa ajiri ya AfyaTshs 10,000/=
C. Bima ya Afya 50,400/= (kwa wanafunzi wasio na Bima ya Afya ya wazazi)
D. Tahadhari Tshs 10,000/=
E. Kitambulisho Tsh 10,000/= (iletwe januari pindi mtoto anaporipoti shuleni)
F. Gharama kwa ajiri kununa mahitajiji madogo madogo ya chakula Tshs 50,000/= kwa muhula (ina lipwa mwezi wa kwanza Tshs 50,000 na mwezi wa saba Tshs 50,000/=)
G. Jembe 01 lenye mpini, na flekeo **(unakuja na kimoja kati ya ivyo )**

***N.B***

***Ada na michango yote*** isipo kuwa rimu na Chakula ***ilipwe benki ya NBC akaunti namba* 023172000141 *jina la akaunti WILOLESI FOUNDATION na iletwe payslip ofisi ya mhasibu wa shule.***

**SARE ZA SHULE**

***I.WAVULANA***

a). Suruali 2 rangi ya blue bahari TSH, 40,000/= (zinapatikana shuleni)
b). Shati rangi nyeupe mikono mifupi 2
c). Sweta la kijani Tshs, 15,000/= (linapatikana shuleni na litawekwa ufito shuleni)
d). T-Shirt yenye nembo ya shule TSH 15000/= (Linapatikana shuleni)
e). Track suit nyeusi
f). Suruali nyeusi (shamba dress) ashone mwanafunzi
g). Viatu vyeusi vya kamba, visigino vifupi jozi 2

**II.WASICHANA**

**a).** Sketi 2 blue bahari Tshs 40,000/= (zinapatikana shuleni, ziwe ndefu na nadhimu kwa maadili ya kitanzania)

**b).** Shati nyeupe mikono mifupi 2

**c).** Sweta rangi ya kijani Tsh 15,000/= (Linapatikana shuleni kuepuka kuwa na rangi tofauti tofauti)

**d).** T-Shirt yenye nembo ya shule Tshs 15,000/= (Linapatikana shuleni)

**e).** Track suit nyeusi

**f).** Sketi nyeusi (shamba dress) ashone mwanafunzi

**g).** Viatu vyeusi vya kamba vyenye visigino vifupi

**h).** Soksi nyeupe.

***AGIZO:***

Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo zingine zozote tofauti na hizi zilizo orodheshwa kwenye fomu hii.

**I.MAHITAJI MENGINE YA MWANAFUNZI**

a). Godoro futi 2.5×6 (zingatia hili kwani vitanda vyetu ni vya ukubwa huo)

b). Shuka rangi ya bluu

c). Chandarua

d). Nguo za ndani za kutosha

e). Viatu vya michezo

g). Bukta na T-Shirt rang ya bluu kwa ajili ya michezo

**I.VIFAA VYA MASOMO**

a). Kamusi ya kiingereza kwa Kiswahili kwa ajili ya kujifunzia Lugha

b). Madaftari ya kutosha yasiyopungua 10 (Counterbook QUIRE 3) ***zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 25000/=***

c). Mathematical set (mkebe) ***unapatikana shuleni***

d). Kalamu za wino za kutosha

e). Rula

**II.VIFAA VYA USAFI**

a). Ndoo ndogo 2

b). Taulo, kitenge kimoja kwa wasichana.

c). Vifaa vingine vya kufanyia usafi wa mwili na mavazi.

**III.VYOMBO VYA MESINI (CHAKULA)**

a). Sahani (trai kwa ajili ya chakula)

b). Kikombe.

HUDUMA NA ELIMU
WILOLESI HEALTH CARE

## MASHARTI NA MAAGIZO MENGINEYO

- Mwanafunzi awe tayari kuheshimu sheria na taratibu za mitihani ya ndani
- Wanafunzi wa kiislamu waje na **hijabu (wasichana), kanzu na kofia (wavulana)** kwa ajili ya sala ya ijumaa tu
- Mwanafunzi haruhusiwi kutunza pesa zaidi ya elfu tano (5000/=) bwenini. Pesa inayozidi kiasi hicho atatunziwa na Mhasibu wa shule
- Mwanafunzi afanyiwe uchunguzi wa afya yake na Daktari

## TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE

## UTANGULIZI

Anayekubali kuwa mwanafunzi wa shule hii sharti akubali kuzingatia kwa makini taratibu na sheria za shule zifuatazo pamoja na sheria ndogo ndogo atakazo ambiwa

## MIPAKA YA SHULE

- Mwanafunzi yeyote awapo shuleni haruhusiwi kwenda nje ya mipaka ya shule mpaka apate kibali kutoka kwa Mkuu wa shule au Mwalimu wa zamu
- Mwanafunzi anapotoka nje ya shule lazima avae sare ya shule na apite kwenye barabara kuu
- Hauruhusiwe kuonekana kwenye nyumba za majirani tofauti na sehemu ulipo elekezwa.

## USAFI

- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujiweka safi yeye mwenyewe na mazingira yake
- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kwenye shughuli za usafi wa shule
- Kila vazi litumike katika muda na mahali kadri ya sheria ndogo zinavyo elekeza

## VYOMBO VYA MUZIKI NA MAWASILIANO

- Haruhusiwi mwanafunzi kuwa na RADIO na vyombo vingine vya MUZIKI
- Ni marufuku mwanafunzi kuwa na SIMU za mkononi, atakayekutwa na simu atarudishwa nyumbani

## WAGENI

- Ni marufuku kumkaribisha, kumtembeza mgeni katika eneo la shule bila kupata kibali toka kwa Mkuu wa shule au Mwalimu wa zamu. Wageni wafike Utawala na wapate maelekezo hapo
- Watu wafuatao wataruhusiwa kumtembelaea mwanafunzi: **Baba, Mama au Mlezi** nani mwisho wa mwezi tu.

## BWENINI

HUDUMA NA ELIMU
WILOLESI HEALTH CARE

- Kelele za aina yoyote bwenini zinakatazwa
- Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchemsha/ kupika au kula chakula bwenini
- Muda wa kulala na kuamka uzingatiwe kwa makini

**DINI**

- Kila mwanafunzi ashike na kuheshimu dini yake
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kudharau au kukashifu dini za Wengine
- Ibada zote za wanafunzi zifanyike kadri ya taratibu za shule

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

Mwanafunzi akitenda kosa lolote kati ya haya yafuatayo atafukuzwa shule:

- Wizi
- Kupata mimba
- Uvutaji wa bangi/ madawa ya kulevya
- Makosa ya jinai
- Kupigana
- Kuoa au kuolewa
- Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa
- Kugoma adhabu ya Mwalimu
- Kubaki bwenini muda usio ruhusiwa
- Ushoga (homosexuality)
- Kuongoza au kushiriki mgomo wa aina yoyote ile
- Kuongoza au kushiriki mkutano usio rasmi/ usio na idhini
- Kutumia simu/ kukutwa na simu mazingira ya shuleni, kukutwa na laini ya simu na karatasi ya Vocha

*Imeandaliwa Na,*

…………………………..

*Mwl. Alex Komba*

***MKUU WA SHULE***

HUDUMA NA ELIMU
WILOLESI HEALTH CARE